



TANZANIA MORTGAGE REFINANCE COMPANY LIMITED (TMRC)

(Imesajiliwa Tanzania chini ya Sheria ya Kampuni, Sura ya 212, Sheria Na. 12 ya mwaka 2002 kama kampuni yenye dhima ndogo – Hati ya Usajili Na. 74792)

TANGAZO KWA UMMA

MATOKEO YA OFA YA HATI FUNGANI YA NYUMBA 'NYUMBA BOND' KWA UMMA NA MGAO

Kampuni ya Tanzania Mortgage Refinance Company Limited (TMRC) inatoa taarifa kwa umma kuwa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA), katika kutekeleza majukumu yake chini ya Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana, Sura ya 79 ya Sheria za Tanzania, mnamo tarehe 28 Aprili 2026 iliidhinisha Waraka wa Taarifa kuhusiana na TMRC toleo la Hati Fungani ya Nyumba yenye thamani ya TZS bilioni 20, ikiwa ni awamu ya kwanza ya Programu ya Hati Fungani za Muda wa Kati (MTN) yenye jumla ya shilingi bilioni 100.

HALI YA OFA

Toleo la Hati Fungani ya 'Nyumba Bond' lilifunguliwa Jumatano, tarehe 06 Mei 2026 na kufungwa Jumatano, tarehe 03 Juni 2026. Baada ya kufungwa kwa toleo hilo, TMRC inafuraha kutangaza kuwa ilipokea maombi ya Hati Fungani yenye thamani ya **TZS bilioni 30.235**, ikilinganishwa na mpango wa awali wa TZS bilioni 20, sawa na kiwango cha mafanikio ya asilimia 151.18.

MATOKEO YA NYUMBA BOND:

Muhtasari wa takwimu muhimu za matokeo ya toleo ("Toleo")

| SN | Kipengele | Maelezo |
|----|--|--|
| 1 | Mtoaji: | Tanzania Mortgage Refinance Company Limited |
| 2 | Jina la Hati Fungani | 'Nyumba Bond' |
| 4 | Tarehe ya Utoaji: | 12 Juni 2026 |
| 5 | Tarehe ya Kukomaa: | 12 Juni 2031 |
| | Muda: | Miaka 5 |
| 6 | Kiasi Kilichotolewa: | TZS 20,000,000,000/- |
| 7 | Kiasi Kilichokusanywa: | TZS 30,235,050,000/- |
| 8 | Kiwango cha Usajili: | 151.18% |
| 9 | Kiasi kilichokubaliwa: | TZS 30,235,050,000/- |
| 10 | Bei ya Utoaji: | 100% (Par) |
| 11 | Riba: | 11% kwa mwaka; itakayolipwa kila baada ya miezi 6 |
| 12 | Kiwango cha Chini cha kuwekeza: | TZS 500,000/- na nyongeza katika mafungu ya TZS 10,000/- |
| 14 | Tarehe za Malipo ya Riba: | 12 Juni na 12 Disemba kila mwaka hadi tarehe ya Ukomavu |
| 12 | Tarehe ya Kuanza kwa Riba | 12 Juni 2026 |
| 15 | Tarehe ya Uorodheshaji: | 06 Julai 2026 |

SERA YA MGAO:

Kutokana na kiwango cha mwitikio cha asilimia 151.18%, TMRC iliomba na kupata idhini kutoka CMSA ya:

- i. Kutumia kiasi chote kilichokusanywa; na
- ii. kukubali maombi yote halali yaliyopokelewa, na hivyo kufanya kiasi kinachopatikana kwa ajili ya mgao kufikia TZS 30,235,050,000/-

Kwa hiyo, waombaji watapokea mgao wa asilimia 100.

UFAFANUZI:

Kwa ufafanuzi zaidi, waombaji wanashauriwa kuwasiliana na dalali wao wa soko la hisa au Tanzania Mortgage Refinance Company Limited (TMRC) kupitia barua pepe: info@tmrc.co.tz au simu +255 (22) 2215100 kuhusu maombi yao.

SHUKRANI:

Menejimenti ya Tanzania Mortgage Refinance Company Limited (TMRC) inapenda kutoa shukrani kwa taasisi zote zilizowezesha mafanikio ya utoaji huu wa kihistoria wa hati fungani. Taasisi hizo ni pamoja na Bodi na Menejimenti ya Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA); Bodi na Menejimenti ya Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE); Washauri Wakuu wa Muamala wa TMRC, Stanbic Bank Tanzania; Wakala Mdamini, Alpha Capital; Mshauri wa Kisheria, Abenry Advocates; Mshauri wa Kifedha, KPMG; na Benki Pokezi, Msajili na Wakala wa Fedha, NMB Bank Plc.

Imetolewa na:

**Afisa Mtendaji Mkuu
Tanzania Mortgage Refinance Company Limited
Ghorofa ya 15, Golden Jubilee - Main Tower,
Mtaa wa Ohio & Kibo,
SLP 7539,
Dar es Salaam, TANZANIA**

TAREHE: 06 Julai 2026

Tangazo hili limetolewa kwa idhini ya Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) kwa mujibu wa Kanuni za Matangazo za Masoko ya Mitaji na Dhamana, Tangazo la Serikali Na. 15 la mwaka 1997.